



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA**

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)



Simu: +255 623 145 188  
Barua pepe: [ded@kyerwadc.go.tz](mailto:ded@kyerwadc.go.tz)  
Tovuti: <http://www.kyerwadc.go.tz>  
Unapojibu tafadhali taja:-

S.L.P 72,  
KYERWA.

Kumb. Na. FG. 740/898/11/57

04/08/2022

## **TANGAZO LA KAZI (LINARUDIWA)**

Kwa mujibu wa kibali cha Ajira Mpya kilichotolewa na Katibu Mkuu – Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa chenye Kumb. Na. FA. 97/228/01/9 cha tarehe 13 Mei, 2022. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa anawatangazia watanzania wenye sifa na uwezo kujaza nafasi ifuatayo:-

### **DEREVA DARAJA LA II – TGS. B (NAFASI 2)**

#### **SIFA ZA MWOMBAJI:**

- i) Aliyefaulu elimu ya Kidato cha nne (IV)
- ii) Awe na leseni ya Daraja la E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali
- iii) Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- iv) Waombaji wenye cheti cha Majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

#### **MAJUKUMU YA DEREVA DARAJA LA II:**

- i) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
- ii) Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- iii) Kufanya matengenezo madogo madogo ya magari
- iv) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- v) Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari za safari
- vi) Kufanya usafi wa magari, na
- vii) Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake

#### **NGAZI YA MSHAHARA:**


Kwa mujibu wa Muundo wa Utumishi na Nyaraka za Serikali.

### **MASHARTI YA JUMLA:**

1. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi kwenye Kijiji chochote ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa.
2. Mwombaji awe na umri kati ya miaka 18 – 45.
3. Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
4. Maombi yote yaambatane na Wasifu wa mwombaji (CV).
5. Maombi yaambatanishwe na nakala za vyeti vya elimu, vyeti vya taaluma, cheti cha kuzaliwa na picha (passport size) zilizoandikwa jina la mwombaji nyuma.
6. Testimonials "Provisional results", "Results slips" kiapo cha kuthibitisha umri wa kuzaliwa HAVITAKUBALIKA.
7. Barua ya maombi iandikwe kwa mkono.
8. Waombaji ambao walisoma nje ya nchi vyeti vyao vya Taaluma vifanyiwe ulinganishi na TCU na NECTA na majibu ya ulinganisho yaambatanishwe kwenye barua ya maombi ya kazi.
9. Waombaji waliowahi kuacha kazi, kuachishwa au kufukuzwa kazi hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama na Kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi cha kuajiriwa tena.
10. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 18/08/2022 saa 9.30 Alasiri.
11. Maombi yote yatumwe kwa:-

**MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA,  
S.L.P 72,  
KYERWA.**

LIMETOLEWA NA;

  
SACF. James M. John  
**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
KYERWA**

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
KYERWA**

Nakala: Mbao za Matangazo.

: Tovuti ya Halmashauri: [www.kyerwadc.go.tz](http://www.kyerwadc.go.tz)

: Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira: [www.ajira.go.tz](http://www.ajira.go.tz)

